# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO, KAZI ZAKE NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA WAKALA


4. Kuanzishwa kwa Wakala.
5. Malengo ya Wakala.
6. Kazi za Wakala.
7. Uwezo wa Wakala.


### SEHEMU YA TATU
### UONGOZI WA WAKALA


8. Bodi ya Ushauri.
9. Sifa za Mwenyekiti.
10. Makamu Mwenyekiti.
11. Katibu wa Bodi.
12. Kazi za Bodi.
13. Muda wa Bodi.
14. Vikao vya Bodi.

15. Uamuzi wa Bodi.

16. Kamati za Bodi.

17. Kujiuzulu kwa Mwenyekiti au mjumbe.

18. Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

19. Posho ya wajumbe.

20. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

21. Kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

22. Idara na vitengo vya Wakala.

23. Wafanyakazi wengine wa Wakala.

**SEHEMU YA NNE**
**MASHARTI YA FEDHA**

24. Fedha na vyanzo vya mapato vya Wakala.

25. Bajeti.

26. Kufungua hesabu ya benki.

27. Hesabu na ukaguzi.

28. Ripoti ya mwaka.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA JUMLA**

29. Uwezo wa Wakala kutaka taarifa.

30. Kinga.

31. Kuhaulisha mali na madeni.

32. Kanuni.

33. Kufutwa na kubakizwa vifungu vya 96 na 97 vya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011.

**SHERIA NAM. 12 YA 2019**

**NIMESAINI**

Alshein

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

31 Disemba......................................, **2019**

## SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA SERIKALI MTANDAO, KAZI ZAKE NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza. kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar ya mwaka 2019 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataiteua kwa kuitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa taasisi zote za umma na watumishi wa umma kwa mambo yanayohusiana na matumizi ya huduma za kieletroniki zinazotolewa na Serikali.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa pale maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar ulioanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Ushauri ya Wakala iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8(1) cha Sheria hii;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8(1) (a) cha Sheria hii, na inajumuisha mtu mwengine yeyote aliyeteuliwa kufanya kazi za Mwenyekiti;

"Serikali mtandao" maana yake ni matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika utendaji wa Serikali na utoaji huduma za umma;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 20(1) cha Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Miundombinu" maana yake ni mfumo na vifaa muhimu vinavyowezesha taasisi za Serikali, watu binafsi na jamii kwa ujumla kupata huduma za serikali mtandao;

"TEHAMA" maana yake ni teknolojia ya habari na mawasiliano, inayojumuisha nyenzo na rasilimali za teknolojia zinazotumika katika kukusanya, kuchakata, kuhifadhi, kusafirisha, kusambaza, na kupata taarifa katika utumishi wa umma;

"Mjumbe" maana yake ni Mjumbe wa Bodi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na mambo ya huduma za Serikali mtandao;

"Taarifa huria" maana yake ni taarifa ambayo iko huru kutumiwa na umma na wanayoweza kuichapisha kama watakavyohitaji, bila vikwanzo kutoka hatimiliki au namna nyengine za udhibiti kwa mujibu wa sheria;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA WAKALA

Kuanzishwa kwa Wakala.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Wakala utakaojulikana kama Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar.

(2) Wakala, baada ya kupata ridhaa ya Waziri, utakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kumiliki, kununua au kuondoa mali inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia kwenye mikataba au miamala yoyote kwa mujibu wa taratibu za kisheria;

(c) kukopa kiasi chochote cha fedha kutoka katika taasisi za fedha kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(d) kufanya au kutenda jambo lolote ambalo kisheria, Wakala kwa asili yake, unaruhusika kufanya au kutekeleza.

(3) Wakala utakuwa na muhuri, nembo na jina fupi kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(4) Matumizi ya muhuri na nembo ya Wakala juu ya waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mtendaji au ofisa mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji.

(5) Waraka wowote ili uwe ni hati iliyotolewa na Wakala, utatakiwa kuwekwa muhuri wa Wakala na kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki.

Malengo ya Wakala.

**5.** Malengo ya Wakala yatakuwa ni:

(a) kuratibu shughuli za serikali mtandao kwenye taasisi za umma na utoaji huduma za Serikali kupitia matumizi ya TEHAMA;

(b) kuhakikisha mifumo ya habari na mawasiliano inawekwa, inaimarishwa na inaendelezwa kwa mujibu wa sera na viwango itakayopelekea kuwa na upashanaji habari mzuri, wenye gharama nafuu utakaorahisisha shughuli za Serikali;

(c) kuhakikisha upatikanaji wa huduma za Serikali nchi nzima kwa urahisi, ufanisi, uthabiti, kwa kutumia mifumo sahihi ya TEHAMA;

(d) kushajihisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma; na

(e) kuwa kitovu cha utaalamu katika kuandaa na kuendeleza sera, viwango na taratibu nyengine kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma Zanzibar.

Kazi za Wakala.

**6.** Kazi za Wakala zitakuwa ni:

(a) kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera za TEHAMA, kanuni na miongozo katika utumishi wa umma;

(b) kusimamia maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma;

(c) kutekeleza maagizo ya kisera na maamuzi mengine ya Serikali kuhusiana na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma;

(d) kuanzisha mifumo ya utekelezaji kwa ajili ya kuwezesha na kuratibu upatikanaji huduma za serikali mtandao;

(e) kushauri mamlaka husika na taasisi yoyote ya umma juu ya matumizi bora ya TEHAMA katika usimamizi na utoaji wa huduma za umma;

(f) kuanzisha, kusimamia na kuendeleza mifumo ya pamoja ya serikali mtandao na huduma;

(g) kuanzisha na kuendeleza mifumo ya taarifa huru kwa ajili ya matumizi ya umma;

(h) kuoanisha, kuratibu na kuendeleza shughuli za serikali mtandao katika taasisi za umma;

(i) kuanzisha na kuendeleza rejista za mifumo ya serikali mtandao na huduma;

(j) kuandaa na kuweka kumbukumbu za wataalamu wa TEHAMA, kupendekeza maslahi na kuratibu matumizi ya wataalamu hao katika utumishi wa umma;

(k) kusimamia miradi ya serikali mtandao inayotekelezwa na taasisi za umma;

(l) kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya kutathmini utendaji kazi wa Serikali Mtandao;

(m)kuthibitisha mifumo ya taarifa inaendana na mahitaji ya mifumo mingine na usalama;

(n) kutumia uwezo chini ya mikataba na makubaliano yaliyokubaliwa na Serikali kuhusiana na masuala ya Serikali Mtandao;

(o) kufanya tafiti na kazi za kimaendeleo kuhusiana na masuala ya serikali mtandao; na

(p) kutekeleza kazi nyengine yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa malengo yake chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Wakala.

**7.** Uwezo wa Wakala utakuwa ni:

(a) kuitaka taasisi ya umma kutoa taarifa kama itakavyohitaji katika kutekeleza kazi zake zilizopo chini ya mamlaka yake;

(b) kutoa maelekezo kwa taasisi ya umma kuhusiana na utekelezaji wa sera za serikali mtandao;

(c) kuidhinisha uanzishaji na uendeshaji wa huduma na mifumo ya kieletroniki katika utumishi wa umma;

(d) kukagua huduma za serikali mtandao katika taasisi za utumishi wa umma; na

(e) kuidhinisha mikakati ya kisekta ya maendeleo ya Serikali ya kielektroniki na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya serikali mtandao.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI WA WAKALA

Bodi ya Ushauri.

**8.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Ushauri ya Wakala ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala;

(c) Mkurugenzi anayehusika na usimamizi wa utumishi wa umma;

(d) Mkurugenzi anayehusika na miundombinu ya TEHAMA;

(e) Mkurugenzi anayehusika na Serikali za Mitaa;

(f) Mtaalamu mmoja wa TEHAMA kutoka taasisi ya umma ya elimu ya juu Zanzibar;

(g) Mtaalamu mmoja mwandamizi wa TEHAMA katika utumishi wa umma; na

(h) Mtaalamu mmoja kutoka Tume ya Mipango.

(2) Isipokuwa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, uadilifu, taaluma na jinsia.

(3) Mjumbe aliyeteuliwa na Waziri chini ya aya (f), (g) na (h) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atasita kuwa mjumbe wa Bodi mara baada ya sifa za uteuzi wake zitakaposita.

Sifa za Mwenyekiti.

**9.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana elimu angalau shahada ya kwanza katika fani ya TEHAMA, sheria, uchumi, fedha, utawala, utumishi wa umma au fani nyengine zinazolingana kutoka katika taasisi inayotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi wa kutosha katika fani zilizoelezwa chini ya aya ya (b) ya kifungu hiki; na

(d) anaheshimika.

Makamu Mwenyekiti.

**10.** Wajumbe wa Bodi, katika kikao cha kwanza, watachagua mjumbe mmoja miongoni mwa wajumbe kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Katibu wa Bodi.

**11.**-(1) Kutakuwa na Katibu wa Bodi atakayeteuliwa na Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana angalau shahada ya kwanza ya sheria na ni mfanyakazi wa Wakala.

Kazi za Bodi.

**12.**-(1) Bodi itakuwa na kazi za:

(a) kushauri juu ya usimamizi wa utendaji wa Wakala;

(b) kumshauri Waziri katika masuala ya maendeleo ya kisera na mikakati inayohusiana na Serikali Mtandao;

(c) kufanya mapitio na kushauri kuhusiana na mipango ya uendeshaji, bajeti, taarifa za utendaji na za ukaguzi wa fedha za Wakala;

(d) kushauri katika kuweka malengo, shabaha na hatua za utekelezaji wa Wakala;

(e) kupendekeza muundo wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(f) kushauri kuhusiana na taratibu na masharti ya utumishi ya wafanyakazi wa Wakala kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(g) kushauri kuhusiana na hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Wakala;

(h) kupendekeza kuhusiana na bajeti ya Wakala; na

(i) kufanya kazi nyengine yoyote iliyopo chini ya Sheria hii au ambayo inaweza kuwa ni muhimu kwa ajili ya kufikia madhumuni ya kuanzishwa kwa Wakala.

(2) Katika utekelezaji wa kazi zake, Bodi itawasilisha taarifa kila robo mwaka kwa Waziri.

Muda wa Bodi.

**13.**-(1) Mwenyekiti atashika madaraka kwa kipindi cha miaka minne kuanzia tarehe aliyoteuliwa na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(2) Ukiacha wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi ya ujumbe wa Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Vikao vya Bodi.

**14.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(2) Bodi inaweza kukutana katika kikao cha dharura wakati wowote itakapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

(3) Taarifa ya maandishi ya kikao cha Bodi itatolewa na Katibu angalau siku saba kabla ya tarehe ya kufanyika kikao.

(4) Vikao vyote vya Bodi vitaitishwa na Mwenyekiti au ikiwa Mwenyekiti hayupo, vitaitishwa na Makamu Mwenyekiti.

(5) Akidi ya kikao itakuwa ni nusu ya Wajumbe wote wa Bodi.

(6) Ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliohudhuria watachagua mjumbe mmoja miongoni mwa wajumbe kuendesha kikao, na mjumbe aliyechaguliwa atakuwa na mamlaka yote na atatekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti kwa kikao hicho.

Uamuzi wa Bodi.

**15.**-(1) Bodi itafanya uamuzi wake kwa njia ya makubaliano na ikiwa makubaliano hayatafikiwa, uamuzi utafanywa kwa kupiga kura na endapo itatokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

(2) Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye sio mjumbe kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi, lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

(3) Kwa kuzingatia masharti mengine ya Sheria hii, Bodi itajipangia utaratibu wake wenyewe ikijumuisha uanzishaji wa kamati za Bodi.

Kamati za Bodi.

**16.** Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha idadi ya Kamati kutekeleza kazi zake kama Bodi itakavyoamua.

Kujiuzulu kwa mwenyekiti au mjumbe.

**17.**-(1) Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kuandika taarifa ya kujiuzulu na kuiwasilisha kwa mamlaka ya uteuzi, na kuanzia tarehe iliyoainishwa katika taarifa au ikiwa tarehe haikuainishwa, kuanzia tarehe iliyopokelewa taarifa na mamlaka ya uteuzi, mjumbe huyo atasita kuwa mjumbe.

(2) Endapo mtu atasita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi, kama itakavyokuwa, kwa sababu yoyote kabla ya kumalizika kwa muda, mamlaka ya uteuzi itateua mtu mwengine kushika nafasi hiyo na mtu huyo aliyeteuliwa atashika nafasi kwa kipindi kilichobaki cha aliyemtangulia.

(3) Endapo mjumbe aliyeteuliwa na Waziri atashindwa kuhudhuria kwenye vikao vitatu mfululizo bila ya sababu ya msingi, Mwenyekiti atamjulisha Waziri kuhusiana na hilo, na Waziri atafuta uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mtu mwengine na mtu aliyeteuliwa atashika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki cha aliyemtangulia.

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

**18.**-(1) Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi, ikiwa mjumbe:

(a) atamaliza muda wa ofisi;

(b) bila ya sababu ya msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi;

(c) atajiuzulu au kwa sababu yoyote, atapoteza sifa za kuwa mjumbe wa Bodi;

(d) hana uwezo wa kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu ya afya ya kimwili au kiakili; au

(e) atafariki.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii yanayohusiana na akidi, uendeshaji wa vikao vya Bodi hautokuwa batili kwa sababu ya nafasi kuwa wazi au kutohudhuria kwa mjumbe yeyote wa Bodi.

Posho ya wajumbe.

**19.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni na miongozo.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**20.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji, ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana elimu angalau shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya kompyuta, teknolojia ya habari au fani nyengine zinazolingana kutoka taasisi inayotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi angalau miaka kumi katika fani zilizotajwa chini ya aya (b) ya kifungu hiki;

(d) anaheshimika; na

(e) ana kiwango cha juu cha uadilifu.

Kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

**21.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala na atakuwa na wajibu wa kusimamia utendaji wa kazi za kila siku na uongozi wa Wakala.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji yatakuwa ni:

(a) kutekeleza sera na programu za Wakala;

(b) kuwasilisha mitazamo ya Wakala kwa Serikali na umma kwa ujumla;

(c) kusimamia vizuri fedha na mali za Wakala;

(d) kupendekeza na kutekeleza mpango mkakati, mipango ya biashara na uendeshaji wa Wakala;

(e) kuhakikisha matumizi bora ya wafanyakazi na rasilimali nyengine;

(f) kuhakikisha viwango vya juu vya nidhamu miongoni mwa wafanyakazi;

(g) kusimamia masuala ya Wakala katika utoaji wa huduma bora na zenye ufanisi;

(h) kuchukuwa hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Wakala;

(i) kuhakikisha kuwa malengo ya Wakala yanafikiwa na Waziri; na

(j) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii kama atakavyopewa na Bodi.

Idara na vitengo vya Wakala.

**22.**-(1) Wakala wanaweza kuanzisha Idara na vitengo kwa idadi na kwa namna kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake baada ya kuidhinishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakuu wote wa Idara wa Wakala watateuliwa na Waziri baada ya kupendekezwa na Bodi na wakuu wa vitengo watateuliwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa kushauriana na Bodi.

(3) Katika kutekeleza kazi za Wakala, kila Mkuu wa Idara na Kitengo atawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Wafanyakazi wengine wa Wakala.

**23.** Kutakuwa na wafanyakazi wengine wa Wakala watakaoajiriwa kwa kuzingatia taratibu na masharti kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na vyanzo vya mapato vya Wakala.

**24.** Fedha na vyanzo vya mapato ya Wakala zitajumuisha:

(a) fedha kama zitakavyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa utaratibu wa ruzuku;

(b) michango halali, misaada, urithi au mikopo inayoweza kupokelewa kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(c) fedha nyengine zozote ambazo zinaweza kupatikana kihalali na Wakala.

Bajeti.

**25.**-(1) Wakala, kabla ya mwaka mpya wa fedha, utaandaa bajeti ya mwaka na kuiwasilisha kwa Waziri kwa mazingatio na kuidhinisha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(2) Waziri ataiwasilisha bajeti ya mwaka ya Wakala Baraza la Wawakilishi katika utaratibu na namna kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Kufungua hesabu ya benki.

**26.** Wakala utafungua hesabu ya benki kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

Hesabu na ukaguzi.

**27.**-(1) Wakala utaweka na kuhifadhi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Mkurugenzi Mtendaji kila mwisho ya mwaka wa fedha, ataandaa au ataagiza kuandaliwa:

(a) taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi cha mwaka wa fedha husika;

(b) taarifa ya mali na madeni ya Wakala hadi kufikia siku ya mwisho ya mwaka wa fedha kwa ajili ya kuwasilishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi mwengine yeyote aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) taarifa nyengine yoyote ya fedha kama ilivyoelezwa na sheria yoyote.

Ripoti ya mwaka.

**28.**-(1) Wakala, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, utawasilishwa kwa Waziri, ripoti ya mwaka inayohusiana na mwaka huo na itajuimisha:

(a) nakala za hesabu za Wakala zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya mkaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) taarifa ya utekelezaji kulingana na shabaha na taarifa nyengine yoyote inayohusiana nayo;

(c) taarifa inayohusiana na utendaji wa Wakala kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha; na

(d) taarifa nyengine yoyote inayohusiana na kazi za Wakala kama Waziri atakavyohitaji.

(2) Waziri atahakikisha kwamba nakala ya ripoti ya mwaka inawasilishwa Baraza la Wawakilishi baada ya kupokea ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Uwezo wa Wakala kutaka taarifa.

**29.**-(1) Wakala unaweza, katika utekelezaji wa kazi zake, kumwita mtu yeyote au taasisi kwa maandishi ambaye ana dhamana na taarifa yoyote inayoweza kuhusiana na kazi ya Wakala na itakuwa wajibu kwa mwenye dhamana na taarifa hiyo kuiwasilisha kwa Wakala isipokuwa kama sheria itazuia kufanya hivyo.

(2) Katika utekelezaji wa mamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Wakala utakuwa na uwezo wa kumwita mtu yeyote au taasisi kutoa taarifa inayohusiana na kazi za Wakala.

(3) Mtu au taasisi inayotakiwa kutoa taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatakiwa kufuata matakwa hayo.

(4) Mtu au taasisi itakayoshindwa au kukataa kufuata matakwa hayo, itakuwa imefanya kosa na ikitiwa hatiani, itawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au vyote viwili faini na kifungo.

Kinga.

**30.** Mjumbe wa Bodi au mfanyakazi wa Wakala hatoweza kushitakiwa yeye binafsi kwa jambo au kitu alichokifanya, ikiwa jambo au kitu hicho amekifanya kwa nia njema kwa ajili ya kutekeleza kazi au mamlaka ya Wakala chini ya Sheria hii au kwa maelekezo ya Waziri.

Kuhaulisha mali na madeni.

**31.**-(1) Mali zote za aina tofauti, ikijumuisha vitu vilivyo chini ya Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano iliyopo ndani ya Wizara inayohusika na utumishi wa umma kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, vitachukuliwa kuwa ni mali za Wakala.

(2) Haki zote, fursa, faida, madeni na wajibu uliokuwa katika Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano iliyoopo ndani ya Wizara inayohusika na utumishi wa umma kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, zitachukuliwa kuwa ni za Wakala.

Kanuni.

**32.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ujumla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni mahsusi kuhusiana na:

(a) mawasiliano ya kielektroniki katika utumishi wa umma;

(b) matumizi ya saini za kielektroniki katika utumishi wa umma;

(c) uanzishaji na uendelezaji wa mifumo ya TEHAMA katika utumishi wa umma; na

(d) udhibiti wa taarifa, na mifumo na huduma za TEHAMA katika utumishi wa umma.

Kufutwa na kubakiza kwa vifungu vya 96 na 97 vya Sheria ya Utumishi wa Umma.

**33.**-(1) Vifungu vya 96 na 97 vya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 2 ya 2011 vinafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano chini ya masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma au sheria nyengine yoyote kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, litaendelea na litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

(3) Wafanyakazi waliopo katika Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Wizara inayohusika na Utumishi wa Umma wataendelea kufanyakazi na watachukuliwa kuwa ni wafanyakazi wa Wakala mara baada ya Sheria hii kuanza kutumika.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 4 Disemba, 2019.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***